**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**121/2** **KISWAHILI 2**

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Jumanne, 14 Februari 2012 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## FASIHI KWA UJUMLA

1. "Mabadiliko mbalimbali katika jamii huelekeza utunzi wa kazi za fasihi." Tumia utanzu wa riwaya kuthibitisha dai hilo kwa kutoa hoja tano.

2. "Tamthiliya huundwa kwa kuzingatia sifa za sanaa za maonesho." Tumia hoja nne kufafanua kauli hii kisha toa mfano wa tukio moja la tamthiliya lenye sifa hizo.

## SEHEMU B (alama 20)

## USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | **Haji Gora** |
| **Mapenzi Bora** | - | **Shaaban Robert** |
| **Chungu Tamu** | - | **Theobald A. Mvungi** |
| **Fungate ya Uhuru** | - | **Mohamed S. Khatibu** |

3. "Ushairi ni sukari tamu ya kumezea dawa chungu ili kutibu ugonjwa sugu." Thibitisha usemi huo kwa kutumia mifano minne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

4. "Mdundo wowote lazima uwe na mlio." Eleza vilio vya wasanii wa diwani mbili ulizosoma kwa kutoa mifano minne kwa kila diwani.

## SEHEMU C (alama 20)

## RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| **Usiku Utakapokwisha** | - | **Mbunda Msokile** |
| **Kufikirika** | - | **Shaaban Robert** |
| **Mfadhili** | - | **Hussein Tuwa** |
| **Vuta N' kuvute** | - | **Shafi Adam Shafi** |

5. "Mwanamke amechorwa katika sura mbalimbali." Zipambanue sura hizo katika riwaya mbili ulizosoma kwa kutoa mifano minne kwa kila kitabu.

6. "Uteuzi mzuri wa mandhari ni kielelezo cha kufanikiwa kwa mwandishi." Thibitisha kauli hii kwa kutumia mifano minne kwa kila kitabu katika riwaya mbili zilizoorodheshwa.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 20)

## TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - | **Ebrahim Hussein** |
| **Morani** | - | **Emmanuel Mbogo** |
| **Kivuli Kinaishi** | - | **Said Mohamed** |
| **Nguzo Mama** | - | **Penina Muhando** |

7. "Mivutano ni sehemu ya maisha ya jamii." Fafanua migogoro minne iliyojitokeza kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili ulizosoma.

8. "Wasanii wa tamthiliya huibua matatizo yanayotokea katika jamii na kuyatolea au kutoyatolea masuluhisho." Fafanua matatizo manne kwa kila kitabu ambayo msanii hakuyatolea masuluhisho katika tamthiliya mbili ulizosoma.

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

9. Soma shairi lifuatalo kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata:

Maisha ya mwanambuzi, si leo tangu kitambo,
Heshiwi mapingamizi, mzingiwa na **ulimbo,**
Wima wima usingizi, mashaka kukimu tumbo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Maisha ya mwanambuzi, thama tuyambe msimbo,
Ni maisha ya **gumbizi**, tena yanuka **shombo,**
Hachani na vizuizi, uchao hula makombo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Mashaka ya mwanambuzi, mbele kamba nyuma fimbo,
Hubembezwa kwa uluzi, mchunga haimbi nyimbo,
Hapati nafasi mbuzi, Kumrarua Kiwambo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Majuto ya mwanambuzi, mwanambuzi hana kombo,
Akikwepa mchuuzi, huwa mchuzi wa kombo,
Mtego wa mlanguzi, kwake mbiu ya mgambo,
Mbele kamba nyumba fimbo, maisha ya mwana mbuzi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Nimefanya uchunguzi, mbuzi mnyonge kwa tambo,
Mbuzi hana uamuzi, maisha yake ni **chambo,**
Yapekue mpekuzi, utadhihiri vigambo,
Mbele kamba nyuma fimbo, Maisha ya mwanambuzi.

Tama hiino mbawazi, kiumbe katika fimbo,
Maisha ya masingazi, mpekecho huo wimbo,
Ziwapi sababu wazi. **Kutitia kwenye lambo,**
Mbele kamba nyuma fimbo maisha ya mwanambuzi.

**Maswali**

(a) Eleza taswira mbili muhimu zinazojitokeza katika shairi hili.
(b) Eleza dhamira zinazopatikana katika shairi hili.
(c) Kwa maneno yasiyozidi matatu andika kichwa cha shairi hili.
(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
  (i) Ulimbo
  (ii) Gumbizi
  (iii) Chambo
  (iv) Shombo
  (v) Kutitia kwenye lambo

(e) Fafanua kwa kifupi muundo wa shairi hili.
(f) Unafikiri mshairi ana ujumbe gani kwa hadhira yake.

10. Soma habari ifuatayo kwa makini, kisha onesha mbinu za kifani zilizotumika:

Siku moja Bwana Maburuki, Suriama mmoja kutoka Usheli aliketi juu ya kiti cha uvivu. Kiti kile alichokikalia Bwana Maburuki kilikuwa umbali wa dhiraa tatu hivi kutoka kwa Hashimu. Kama vile amelewa kwa ufahari wake, Bwana Maburuki, akivuta buruma huku akitingisha guu, alimkita jicho la dharau Hashimu, ambaye ingawa ni hirimu yake lakini ni maskini na yu mtumishi wake wa dukani wa miaka nenda rudi. Duka lilikuwa duka hasa, si kiduka mkoba. Lilisheheni kila aina ya bidhaa, kuanzia kanga za Makenzi, vitambaa vya hariri na mali kadha wa kadha.

Wakati wote huo, Hashimu alikuwa akishughulika kwa mikogo kama aliyehodhi duka, huku akisikiliza watu wanaoomba aheri za bei za bidhaa na kujibishana nao, "Biashara haigombi, mteja ni mfalme." Hashimu alipoiba jicho kwa Bwana Maburuki mboni za Hashimu zikakutana na zile za Bwana Maburuki sawia. Hashimu alitaharuki kwa jicho la Bwana Maburuki na bila ya kusita akauliza, "Kulikoni leo Mahabubu? Mbona umenikazia macho hivyo mithili ya kungwi anayemfunda mwali kwa ishara?"

"Hakuna kitu ila tu fahari bila mali muhali." Maburuki alijibu huku akitoa tabasamu la dharau kama ilivyo kawaida yake, ya kuwanyanyasa wanyonge na kuwaweka kwenye kiganja. "Naam, muhali." Hashimu alijibu. "Lakini" akaendelea, "Mali bila daftari hughibu bila ya habari."



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

"Kumbe ndiyo maana faida, haramu, haipatikani kwa sababu fedha zote unapeleka kwenu," Maburuki alifoka huku kidazi kikimvuja jasho. Mzozo ukaanza papo hapo na Hashimu na Bwana Maburuki wakaanza kunyosheana vidole.

"Umeniambia msungo," Maburuki akashutumu.
"La hasha," Hashimu akakana, Unaniiba kauli."

Alimuradi pakawa na zogo mtindo mmoja. Ikazuka hekaheka vitanda na mkeka. Bidhaa zikazagaa mchafukoge hapo dukani. Watu nao kama ujuavyo hawana dogo. Wakaanza kumiminika kama kumbikumbi wa masika. Wakati huo huo Hashimu ambaye alikwishaanza kugonga bati kichwani kutokana na umri wake, akawa anapumua kama mtu aliyefukuzwa na nyati aliyejeruhiwa. Huku akipiga chafya, kwa hasira, maneno yakawa yanamtoka kama cherehani. Usingalijua kama ni yule Hashimu mwenye kigugumizi kwa jinsi alivyokuwa ana sema kama chiriku. "Mungu hawezi kumjalia kila mtu. Aliyekupa wewe kiti, ndiye aliyenipa mimi kumbi." Hashimu alitanabahi huku akipepesa macho yake huku na huko. Hakuonesha uso wa soni.

Kwa kuwa nazi haiwezi kushindana na jiwe, haukupita muda, kwa kuchelea kumwaga unga, japokuwa kazi yenyewe mshahara tonge, Hashimu akaanza kupiga magoti akaomba msamaha kwani ulimi hauna mifupa.

"Lo, Masalale!" Maburuki akavimba kichwa na kuzidi kutamba, kwa kusema, "Nitakushitaki hadi bati kuoza." Maburuki alizidi kumimina kashifa mpaka Hashimu akawa anaomba kimoyomoyo asije akafukuzwa kazi. Ingawa mali si yake, Hashimu ameota kitambi, kama ujuavyo mtegemea nundu haachi kunona na anayekaa karibu na waridi haachi kunukia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org